**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

# TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 16/02/2022 KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

- Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Siha,
- Mwakilishi Ofisi ya RAS-Mkoa wa Kilimanjaro,
- Mh. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Siha,
- Mhe. Makamu Mwenyekiti Halmashhauri ya Siha
- Waheshimiwa Madiwani,
- Ndugu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Siha (Katibu wa Baraza),
- Wah Viongozi wa Madhehebu ya Dini,
- Wageni Waalikwa,
- Ndugu Wataalamu,
- Waandishi wa Habari,
- Wananchi wa Wilaya ya Siha,
- Mabibi na Mabwana,

Napenda kumshukuru Mungu tena kwa mwaka huu mpya wa 2022, Naomba kabla sijaendelea kutoa taarifa yangu katika Baraza hili tukufu la Wah Madiwani naomba tusimame kwa dakika moja na kuwakumbuka wale wenzetu wote waliotangulia mbele za haki kwa mwaka 2022

Nawasalimu wote kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ………..Kipekee napenda kumshukuru Mungu sana kwa ajili ya mshikamano na umoja unaoendelea kushamiri kati ya Viongozi na Wananchi,pia kati ya Wananchi na Wananchi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Siha.

Aidha, kwa nafasi ya kipekee napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali yetu ya awamu ya Sita inayoongozwa na **mhe.SAMIA SULUHU HASSAN** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyofanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa Wananchi wa Tanzania wanapata maendeleo ya kweli hususani katika kuboresha utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Vile vile napenda kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi (CCM) kwa jinsi kinavyoendelea kusimamia Serikali iliyopo madarakani na kuhakikisha

kuwa wananchi wanapata huduma bora na tena kwa haraka bila upendeleo wala ubaguzi wa aina yoyote.

Aidha, napenda pia kuwashukuru **Wah. Madiwani wote** wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa ushirikiano wenu wa dhati na jinsi mnavyoshiriki katika kuhamasisha shughuli za maendeleo katika Kata zenu.

Napenda kuwashukuru Wananchi,Viongozi na Watumishi wote katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa jinsi mnavyoendelea kuunga mkono juhudi za Rais wetu **mama Samia Suluhu Hassan** za Kuhakikisha kuwa Tanzania inabadilika na kupata maendeleo ya kweli kwa kila mmoja wetu kushiriki katika ujenzi wa uchumi kwa kipato cha Familia na Taifa kwa ujumla.

**Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,**

Kama mnavyojua katika kipindi cha robo ya Pili Serikali yetu ya awamu ya Sita chini ya Rais wetu mpendwa **mhe. SAMIA SULUHU HASSAN** imeleta fedha nyingi za maendeleo hususani katika Sekta ya afya na elimu. **Katika mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya uviko-19** Serikali yetu ya Mama SAMIA ilitoa shilingi milioni 640 kwa ajili ya kujenga madarasa 32 yakiwemo 18 ya shule

za Sekondari na 14 ya shule za msingi. Kwa taarifa nimeambiwa kuwa kazi hii imekamilika ambapo katika fedha hizo za madarasa zimejengwa pia ofisi 09 shule za sekondari na 7 shule za msingi ambapo madarasa yaliyojengwa yameanza kutumika katika kuwapokea watoto mwaka huu mpya wa 2022. Hata hivyo napenda kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji na Wataalam wake kwa usimamizi mzuri wa kazi hii kubwa na nzuri kwa Halmashauri yetu na ubora wa ujenzi wa madarasa yaliyojengwa umekuwa mfano bora ndani na nje ya Mkoa wetu wa Kilimanjaro.

Katika fedha hizi pia tumeshuhudia miongoni mwa fedha za tozo zilizotolewa na Serikali yetu kiasi cha shilingi milioni 250 zikiendelea kujenga kituo cha afya Kata ya Orkolili hii yote ni jitihada za Rais wetu mpendwa mama SAMIA SULUHU HASSAN anavyoendelea kuupiga mwingi katika miradi ya maendeleo….**MAMA SAMIA HOYEEEEEEEEE**

**Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,**

Katika taarifa yangu hii fupi yapo mambo machache ambayo nimeona niyazungumzie kama sehemu ya kusisitiza katika mwaka huu mpya wa 2022 ikiwa pia tupo nusu ya mwaka wa fedha 2021/2022. Miongoni mwa masuala machache yaliyopo katika taarifa yangu ni pamoja na suala la

**Ukusanyaji wa Mapato,Utunzaji wa Mazingira,Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo,Utoaji wa huduma kwa jamii pamoja na masuala mengine muhimu kwa jamii yetu**

## A. UKUSANYAJI WA MAPATO

**Waheshimiwa Madiwani, Ndugu Wananchi na Wanahabari**

Kama ilivyo ada taarifa yangu imekuwa ikiendelea kuhimiza na kusisitiza kuhusu umuhimu wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kama muhimili mkuu wa uendeshaji wa shughuli za Halmashauri na uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa jamii yetu. Bado naendelea kutoa wito kwa Watumishi wa Halmashauri kufuatilia kwa karibu zoezi la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuzingatia sheria ndogo tulizonazo katika Halmashauri yetu pamoja na kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya Halmashauri kama vingi vilivyoibuliwa na Wah. Madiwani.

Naomba sana Idara ya fedha na Kitengo cha Mapato kuhakikisha kuwa wanafuatilia kwa karibu na kukusanya mapato yote stahiki ya Halmashauri bila kupoteza hata kidogo. Kwa hili naomba tena kuhimiza usimamizi wa **Stendi ya KIA bado haujafikia katika** viwango vya kutosha nna hivyo bado magari hayaingii stendi na Halmashauri yetu inaendelea kupoteza

mapato katika chanzo hiki muhimu, naomba kuiagiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kuendelea kuweka mikakati ya kuboresha namna bora ya kudhibiti magari ambayo hayaingii stendi ya KIA pamoja na Stendi nyingine zilizopo katika Halmashauri yetu kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo napenda kupongeza jitihada za dhati za Mkurugenzi Mtendaji za kufanya maboresho katika Stendi ya KIA na kutimiza agizo la Kamati ya fedha uongozi na mipango la kufanyia maboresho Stendi ya KIA ambapo sasa kazi imeonekana nzuri kilichobaki ni kuhakikisha magari yanaingia ndani na kuongeza mapato ya Halmashauri.

Wah. Madiwani wamekuwa wakilalamikia na kushauri kuwa bado ukusanyaji wa mapato katika ushuru wa madini na mazao ya misitu kuna upotevu mkubwa sana. Naomba kutoa wito kwa wataalam wanaohusika na mapato kubadilika na kuhakikisha kuwa wanafanya kazi yao kwa uadilifu mkubwa na kuepuka kuwa na tamaa na fedha za umma. Sisi kama Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Siha hatutakuwa na msamaha wala huruma kwa mtumishi yeyote atakayebainika kuhujumu na kutumia fedha za Serikali kwa maslahi yake binafsi.

**B. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Wah. Madiwani na Ndugu Wananchi na Wanahabari**

Katika kipindi cha robo ya pili shughuli ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Siha umeendelea kufanyika kwa fedha nyingi tulizopokea kutoka Serikali yetu ya Tanzania chini ya **mhe. SAMIA SULUHU HASSAN**. Miongoni mwa miradi tuliyoetekeleza ni ujenzi wa madarasa katika shule za Msingi na Sekondari ambapo jumla ya madarasa 32 yamejengwa kama nilivyoeleza awali hapo juu katika taarifa hii ,Tunayo miradi ya afya inayoendelea kama ujenzi wa wodi tatu katika Hospital ya Wilaya ya Siha ambapo Serikali ilitoa shilingi milioni 500,Pia ujenzi wa nyumba moja itakayotumika na Watumishi watatu katika Zahanati ya Roseline kwa gharama ya shilingi milioni 90 ,Pia ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Orkolili unaoendelea kwa gharama ya shilingi milioni 250.

Kutokana na Halmashauri yetu kupokea fedha nyingi kutoka Serikali yetu ya awamu ya Sita,naomba kutoa wito kwa wananchi wa maeneo mbalimbali yaliyopata fedha za miradi ya maendeleo kuendelea kujitoa

katika nguvu kazi na kusimamia matumizi bora na yenye kutoa thamani halisi ya fedha katika ujenzi wa miradi katika maeneo yao.

NB. Kwenye fedha za miradi ya maendeleo naomba kutoa shukrani za dhati na za pekee kwa **mhe. Dkt. Godwin Mollel** Mbunge wa jimbo la Siha na Naibu Waziri wa afya kwa jitihada zake kubwa za kutuwakilisha vema na kuhakikisha Halmashauri yetu inapata fedha za maendeleo. Sisi kama Baraza la Wadiwani tunaahidi kuendelea kushirikiana naye bega kwa bega katika kuchochea na kuharakisha maendeleo ya Wilaya ya Siha.

**Waheshimiwa Madiwani,Ndugu Wananchi na Wanahabari**

Vilevile napenda kutoa wito kwa Viongozi na Wananchi wa Wilaya ya Siha kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa uviko -19 na kuwaomba wananchi kupata chanjo ya ugonjwa huu ambao umekuwa tishio kwa dunia nzima. Naomba kuwashauri wananchi na Viongozi kupuuza taarifa za upotoshaji zinazotolewa na watu wenye nia mbaya kuhusu chanjo ya uviko-19.

**Waheshimiwa Madiwani ,Ndg Wananchi na Wanahabari**

## C. KUHUSU UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Napenda kutoa rai kwa Wananchi na wakazi wa Halmashauri ya Siha kuhakikisha kuwa tunapanda miti ya matunda, mbao na kivuli katika maeneo yetu ya makazi ,katika mashamba yetu na kandokando ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha kuwa tunatunza uoto wa asili ambao unaelekea kutoweka katika maeneo mengi ya Nchi yetu ikiwemo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Siha.

Naomba kutoa agizo kwa idara ya mazingira katika Halmashauri yetu kuhakikisha kuwa inatoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuepuka kulima kando kando ya mito na chemichemi za maji ambazo ndiyo chanzo cha maji kwa Wananchi wetu. Naomba kumwomba Mkuu wetu wa Wilaya ya Siha kutusaidia katika jambo hili kwani yeye anavyo vyombo vingi vya kufanya kazi katika ufuatiliaji. Naomba pia ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia Watendaji wa Kata na Vijiji wasimamie suala la mazingira kwa ukaribu zaidi ili kufanya Wilaya ya Siha kuwa mfano bora katika utunzaji wa mazingira jambo ambalo litasaidia kuongeza shughuli za utalii kupita katika Wilaya.

**Wah Madiwani ,ndugu Wananchi**

Kabla sijafika mwisho wa Taarifa yangu,kama mnavyojua wakati huu tunajiandaa na msimu mkubwa wa kilimo hivyo naomba kutoa wito kwa wananchi wetu kuendelea na shughuli za kilimo na kuzingatia ushauri mbalimbali wa wataalam wa kilimo ili kuweza kupata mavuno ya kutosha na kuinua kipato cha Familia zetu,jamii na Taifa kwa ujumla. Napenda vilevile kutoa agizo kwa Wataalam wa Kilimo na mifugo waliopo katika Kata zetu na Vijiji waendelee kutoa ushauri kwa wananchi wetu kama ilivyo dhamira ya Serikali ya kuwapa ajira na kuwapangia karibu na wananchi.

Mwisho Kabisa napenda kutoa shukrani tena kwa makundi yafuatayo:-

ii)Kwanza kabisa kwa Naibu waziri wa afya na Mbunge wetu wa jimbo la Siha **mhe. Dkt. Godwin Mollel** kwa jitihada zake kubwa za kufanya ufuatiliaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Wilaya yetu.

iii)Pili kwa Mkuu wetu wa Wilaya ya Siha kwa namna anavyojitolea katika kutatua changamoto mbalimbali za Halmashauri zinapojitokeza mfano mzuri ni ule wa stendi ya KIA na mengine mengi uliyoyafanya katika muda huu mfupi uliokuwepo Siha.

iii)Pia napenda kuwashukuru Viongozi wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Wilaya ,Kata na ngazi za mashina kwa namna wanavyoendelea kutoa ushirikiano wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya **CCM 2020-2025**

**Wah Madiwani ,ndugu Wananchi**

Mwisho,napenda nichukue fursa hii kuwashukuru tena Wah. Madiwani wenzangu pamoja na watumishi wa Serikali katika Halmashauri ya Siha kwa jinsi mnavyochapa kazi kwa kujituma,naomba ushirikiano uliopo uendelee daima siku zote kwa maendeleo ya Wananchi wa Wilaya ya Siha. napenda kuwashukuru tena Wananchi na Wakazi wa Siha kwa usikivu wenu mkubwa mlionesha tangu mwanzo wa taarifa yangu hadi sasa ninapohitinisha taarifa yangu, naomba usikivu na utulivu huu uendelee hadi mwisho wa Mkutano wetu na hatimaye tumalize na kuagana kwa upendo na furaha.

**Mungu ibariki Tanzania,Mungu ibariki Wilaya yetu ya Siha**

Asanteni sana kwa kunisikiliza

**Imetolewa na:**

**Mhe. Duncan B. Urassa**

Mwenyekiti wa Halmashauri (W)

**SIHA**